# »Ufugaji w a bata aina ya muscovy«

Bata aina ya muscovy wana rangi nyeupe, nyeusi, kahawia na kijivu na wana uvimbe mwekundu karibu na macho na midomo. Bata hawa ni wa kijamii, na tofauti kati ya dume na jike hupatikana wakiwa wamekomaa.

Madume hunenepa mwili zaidi ya majike hadi kilo 4 kwa dume na kilo 2 kwa jike. Dume pia hutoa sauti laini na hawawezi kupiga mlio. Bata hawa wana miguu yenye kucha na huruka kwa urahisi, hutaga hadi mayai 60 kwa mwaka na wana kipindi cha siku 33–35 za kulalia mayai.

## Usimamizi wa bata aina ya muscovy

Kwanza, hulishwa kulingana na hali ya kimwili na awali, walishe chakula kilicho na asilimia 20% ya protini kwa wiki 3 za kwanza. Kisha wape chakula kilicho na 18% ya protini hadi watakapochukuliwa sokoni kuuzwa. Katika hatua ya kuzaliana wape chakula kilicho na asilimia 16% ya protini, na kisha uwape malisho yenye kalsiamu .

Watolee nafasi ya inchi 6 kwa kila bata, na chakula kilicho na fumuele ili kuepuka kubadhiri chakula. Fuga dume moja kwa majike 7 ili kuruhusu ndege kujamiiana kwa njia ya asili. Hakikisha wanataga mayai kwenye masanduku ya kutotoleshea kwa muda wa siku 35 katika halijoto ya nyuzijoto 27 na unyevu wa 75%. Watolee vyanzo vya maji ili kudhibiti halijoto.

Kwa vile bata hustahimili joto, punguza mafadhaiko ndani ya banda na jenga banda kwa mwelekeo wa mashariki -magharibi na paa iliyopanuliwa ili kupunguza mwanga wa jua. Sehemu ya kutotoleshea iwe na vizimba vya nyavu vilivyojengwa futi 1 kutoka sakafu ili kurahisisha usafishaji.

Vizimba vinapaswa kupashwa joto hadi nyuzijoto 10 kwa kutumia

mishumaa na taa za umeme. Baada ya wiki 3, hamishia vifaranga kwenye banda lililo na matandiko pamoja na sakafu ya saruji. Hakikisha kwamba matandiko ni makavu ili kuzuia ukuaji wa ukungu na viini vya magonjwa. Safisha banda angalau mara moja kila baada ya wiki 2 na uandae kiota kwa kila bata.

Hatimaye, hakikisha kuna hatua za usalama za kuzuia wadudu na magonjwa.